**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAHAKAMA YA KADHI NAM. 9 YA 2017 NA KUTUNGA SHERIA YA MAHAKAMA ZA KADHI NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


| VIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| | **SEHEMU YA KWANZA**<br>**MASHARTI YA AWALI** |
| 1. | Jina fupi na kuanza kutumika. |
| 2. | Ufafanuzi. |
| | **SEHEMU YA PILI**<br>**KUANZISHWA NA MAMLAKA YA MAHAKAMA ZA KADHI** |
| 3. | Kuanzishwa Mahakama za Kadhi. |
| 4. | Muhuri wa Mahakama. |
| 5 | Mamlaka ya awali. |
| 6. | Mamlaka ya eneo. |
| 7. | Mamlaka ya rufaa. |
| 8 | Marudio. |
| 9. | Mapitio. |
| 10. | Rufaa. |
| 11. | Kufuatwa uamuzi wa Mahakama Kuu. |
| 12. | Kadhi anayesikiliza shauri katika Mahakama ya Kadhi. |
| 13. | Sheria ya Ushahidi. |

## SEHEMU YA TATU
## MAAFISA WA MAHAKAMA ZA KADHI


14. Maafisa wa Mahakama za Kadhi.

15. Uteuzi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

16. Sifa za Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

17. Uteuzi wa Kaimu Kadhi Mkuu.

18. Majukumu ya Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

19. Muda wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

20. Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

21. Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa

22. Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Wilaya.

23. Mrajis wa Mahakama za Kadhi.

24. Majukumu ya Mrajis.


## SEHEMU YA NNE
## UTATUZI WA MIGOGORO


25. Uwezo wa Mahakama ya Kadhi kuupeleka mgogoro kwenye utatuzi.

26. Haki za wadaawa katika usuluhishi au upatanishi.

27. Usiri

28. Muda wa usuluhishi au upatanishi.

29. Usitishaji wa usuluhishi au upatanishi.

30. Kufikia mwisho kwa usuluhishi au upatanishi.

31. Usajili wa makubaliano ya utatuzi.

32. Kushindwa kufikia utatuzi kwa njia ya usuluhishi au upatanishi.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

33. Bajeti na fedha za Mahakama za Kadhi.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

34. Uwezo wa Mahakama za Kadhi kutilia nguvu fatwa za Mufti Mkuu.

35. Uwezo wa kutoa amri ya muda mfupi.

36. Mthibitishaji nyaraka na Kamishna wa viapo.

37. Mgongano wa maslahi.

38. Lugha ya Mahakama za Kadhi.

39. Kudharau Mahakama ya Kadhi.

40. Kuhudhuria kwa Wakili, Vakili au Wakala.

41. Kinga ya maafisa wa Mahakama ya Kadhi.

42. Kanuni.

43. Marekebisho ya Jadweli.

44. Kufuta na kubakiza.

## JADWELI

**SHERIA NAM. 8 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

1 Februari, **2024**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAHAKAMA YA KADHI NAM. 9 YA 2017 NA KUTUNGA SHERIA YA MAHAKAMA ZA KADHI NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mahakama za Kadhi, 2023 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais na kwa tarehe itakayotangazwa na Waziri katika Gazeti.

Ufafanuzi.

**2**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"amri ya muda mfupi" maana yake ni zuio la muda mfupi au amri ya muda mfupi inayotolewa kwenye kesi ambayo bado inaendelea;

"Jaji Mkuu" maana yake ni Jaji Mkuu wa Zanzibar;

"Kadhi" maana yake ni Kadhi Mkuu, Kaimu Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu, Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa, Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa au Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Wilaya;

"Kadhi Mkuu" maana yake ni Kadhi Mkuu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria hii;

"Kafala" maana yake ni kuasili mtoto kwa mujibu wa misingi ya Sharia ya Kiislamu;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"mali ya pamoja iliyopatikana wakati wa ndoa" maana yake ni mali iliyopatikana kwa pamoja na wanandoa kutokana na mchango halisi wa kila mmoja wao wakati wa ndoa;

"Mahakama ya Kadhi" maana yake ni Mahakama yoyote kati ya Mahakama za Kadhi zilizoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Mahakama za Kadhi" inajumuisha Mahakama zote zilizoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"mchango halisi" maana yake ni mchango katika mali uliyotolewa moja kwa moja na mwanandoa au kwa niaba ya mwanandoa wakati wa ndoa;

"Mdaawa" maana yake ni mdai, mdaiwa, mkata rufaa au mpinga rufaa kwenye shauri lilokuwepo katika Mahakama ya Kadhi;

"Mrajis" maana yake ni Mrajis wa Mahakama za Kadhi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 23 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Sharia ya Kiislamu" maana yake ni mfumo wa kisheria wa Kiislamu ambao msingi wake ni Qur-an, Hadith, Ijmaa, Qiyas na vyanzo vyengine ya Sharia ya Kiislamu;

"Tume ya Utumishi ya Mahakama" maana yake ni Tume ya Utumishi ya Mahakama iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 102 cha Katiba;

"Ulamaa" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya masharti ya Sheria ya Mufti, Nam. 4 ya 2021;

"upatanishi" maana yake ni njia ya utatuzi wa migogoro ambayo inawashirikisha wadaawa wenyewe kwa msaada wa mtu mwengine kama mshauri;

"usuluhishi" maana yake ni njia ya utatuzi kwa kuwepo wa migogoro ambayo inawashirikisha wadaawa wenyewe mbele ya mtu mwengine kama msuluhishi;

"Vakili" ina maana kama ilivyotafsiriwa chini ya masharti ya Sheria ya Mawakili, Nam. 1 ya 2020;

"Wakala" maana yake ni mtu mwenye hati ya uwakala ambaye anahudhuria katika shauri kwa niaba ya mdaawa kwa ruhusa ya Mahakama;

"Wakili" ina maana kama ilivyotafsiriwa chini ya masharti ya Sheria ya Mawakili, Nam. 1 ya 2020;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya kisheria.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA NA MAMLAKA YA MAHAKAMA ZA KADHI

Kuanzishwa Mahakama za Kadhi.

**3**.-(1) Kunaanzishwa Mahakama za Kadhi zifuatazo:

(a) Mahakama ya Kadhi ya Wilaya;

(b) Mahakama ya Kadhi ya Mkoa; na

(c) Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

(2) Mahakama ya Kadhi ya Mkoa na Mahakama ya Kadhi ya Wilaya zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitakuwa katika kila Mkoa na Wilaya kwa mpangilio wake.

Muhuri wa Mahakama.

**4**. Mahakama za Kadhi zitakuwa na muhuri utakaokuwa na umbo la mahakama kwa namna itakavyoidhinishwa na Jaji Mkuu.

Mamlaka ya awali.

**5**.-(1) Mahakama za Kadhi zitakuwa na mamlaka ya awali ya kipekee ya kusikiliza shauri kwa mara ya kwanza kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

(2) Mamlaka ya awali ya kipekee yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yatatumika baina ya wadaawa ambao ni waislamu.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, mtu yeyote ambaye sio muislamu anaweza kuwasilisha madai katika Mahakama ya Kadhi dhidi ya muislamu, au anaweza kufunguliwa madai dhidi yake na muislamu katika Mahakama ya Kadhi kwa jambo lolote ambalo Mahakama ya Kadhi ina mamlaka nalo.

Mamlaka ya eneo.

**6**.-(1) Mahakama ya Kadhi ya Wilaya au Mahakama ya Kadhi ya Mkoa itakuwa na itatekeleza mamlaka ya kusikiliza shauri katika eneo husika ndani ya Wilaya au Mkoa.

(2) Mahakama ya Kadhi ya Rufaa itakuwa na itatekeleza mamlaka ya rufaa katika eneo lote la Zanzibar.

Mamlaka ya rufaa.

**7**.-(1) Mahakama ya Kadhi ya Mkoa itakuwa na uwezo wa kusikiliza na kuamua rufaa kutoka katika Mahakama ya Kadhi ya Wilaya, na rufaa kutoka katika Mahakama ya Kadhi ya Mkoa zitawasilishwa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

(2) Katika kutekeleza uwezo wake wa rufaa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mahakama ya Kadhi ya Mkoa au Mahakama ya Kadhi ya Rufaa inaweza, pamoja na maelekezo ya muendelezo wowote wa ziada wa kesi kama itakavyoona inafaa:

(a) kukubaliana, kugeuza au kubadilisha hukumu, uamuzi au amri ya Mahakama ya Kadhi ya Wilaya au ya Mahakama ya Kadhi ya Mkoa kama itakavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria; au

(b) kubatilisha na kuamrisha kusikilizwa tena shauri lolote lililosikilizwa na kuamuliwa na Mahakama ya Kadhi ya Wilaya au Mahakama ya Kadhi ya Mkoa kama itakavyoona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(c) kuelekeza kufanyika kwa mapitio ya rufaa itakayoamuliwa na Makadhi wasiozidi watatu kabla ya rufaa hiyo kupelekwa Mahakama Kuu.

Marudio.

**8**. Mahakama ya Kadhi ya Rufaa inaweza, kutokana na ombi au yenyewe ikiamua, kuitisha kumbukumbu za shauri lolote kwa ajili ya kuchambua na kufanya marudio ya mwenendo wa mashauri ya Mahakama ya Kadhi ya Wilaya au Mahakama ya Kadhi ya Mkoa na kutoa amri katika shauri hilo kama inavyoona inafaa ikiona kwamba Mahakama ya Kadhi ya Wilaya au ya Kadhi ya Mkoa:

(a) imetekeleza mamlaka ambayo haikupewa na sheria;

(b) imeshindwa kutekeleza uwezo ambao imepewa; au

(c) imetekeleza mamlaka yake isivyo halali au imetekeleza kimakosa.

Mapitio.

**9.**-(1) Mtu ambaye hakuridhika na uamuzi au amri ya Mahakama ya Kadhi na hakukata rufaa ndani ya siku thelathini, anaweza kuomba kufanyiwa mapitio ya hukumu au amri katika Mahakama hiyo endapo kuna:

(a) jambo jipya na muhimu limegundulika au ushahidi ambao baada ya uchunguzi wa kina, muombaji hakuwa na uelewa wa jambo hilo au hakuweza kuuleta ushahidi huo wakati wa kutolewa uamuzi au amri;

(b) makosa ya kiuandishi au kimahesabu au kosa lililowazi kwenye kumbukumbu; au

(c) sababu nyengine yoyote ya msingi.

(2) Mahakama inaweza kulikubali au kulikataa ombi au kutoa amri nyengine kama inavyoona inafaa.

Rufaa.

**10.**-(1) Mtu ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa, anaweza kuwasilisha rufaa Mahakama Kuu.

(2) Katika kutekeleza mamlaka yake ya rufaa chini ya masharti ya Sheria hii, rufaa itasikiliizwa na Jaji wa Mahakama Kuu ambaye ni muislamu mwanamme, na Ulamaa wanne ambao kwa pamoja, watajulikana kama wajumbe wa Mahakama.

(3) Ulamaa waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, watateuliwa na Jaji Mkuu kwa kushauriana na Kadhi Mkuu.

(4) Katika uteuzi wa Ulamaa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Jaji Mkuu anaweza kuzingatia madhehebu ya wadaawa.

(5) Jopo la Mahakama Kuu wakati wa kusikiliza rufaa, linaweza kumualika mtu yeyote ambaye anaelewa jambo husika kama Mtaalamu wa Mahakama.

(6) Uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusiana na rufaa hiyo utazingatia maoni ya wajumbe wengi.

Kufuatwa uamuzi wa Mahakama Kuu.

**11.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Katiba, uamuzi wa Mahakama Kuu utakuwa ni wa mwisho.

(2) Uamuzi wa Mahakama Kuu unaohusiana na shauri lililotoka katika Mahakama za Kadhi utalazimika kufuatwa na Mahakama za Kadhi zote lakini katika kutumia uamuzi huo kama rejea, madhehebu ya wadaawa yatatakiwa kuzingatiwa.

Kadhi anayesikiliza shauri katika Mahakama ya Kadhi.

**12.**-(1) Mahakama ya Kadhi itaongozwa na Kadhi husika kwa mujibu wa mamlaka ya Mahakama hiyo katika mambo yaliyoainishwa kusikilizwa na Mahakama hiyo.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kadhi ambaye anasikiliza shauri ataweka kumbukumbu za mwenendo wa mashauri kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa.

Sheria ya Ushahidi.

**13**. Mahakama ya Kadhi, katika kutekeleza mamlaka yake, itatumia sheria na kanuni za ushahidi za Sharia ya Kiislamu.

## SEHEMU YA TATU
## MAAFISA WA MAHAKAMA ZA KADHI

Maafisa wa Mahakama za Kadhi.

**14**.-(1) Mahakama za Kadhi zitakuwa na maafisa wa Mahakama wafuatao:

(a) Kadhi Mkuu;

(b) Naibu Kadhi Mkuu;

(c) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa;

(d) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa;

(e) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi wa Wilaya; na

(f) Mrajis wa Mahakama za Kadhi.

(2) Ukitoa Maafisa wa Mahakama waliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, waajiriwa wengine wa Mahakama za Kadhi watakuwa ni watumishi wengine wasiotekeleza kazi za uamuzi.

Uteuzi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

**15**.-(1) Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Makadhi au mtu ambaye ana sifa ya kuteuliwa kuwa Kadhi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Tume ya Utumishi ya Mahakama, itapendekeza kwa Rais majina ya watu ambao wana sifa ya kuteuliwa kuwa Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu.

(3) Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu watalipwa mishahara na mafao mengine kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Nam. 11 ya 2018.

Sifa za Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

**16**. Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ni muumini na mfuasi wa dini ya Kiislamu;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya Sharia ya Kiislamu kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali au mtu ambaye ni mbobezi katika Sharia ya Kiislamu;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka saba katika mambo yanayohusiana na Sharia ya Kiislamu; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Uteuzi wa Kaimu Kadhi Mkuu.

**17.**-(1) Rais anaweza, endapo Kadhi Mkuu ameshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na sababu za kiafya au sababu nyengine yoyote, na baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kumteua Naibu Kadhi Mkuu kuwa Kaimu Kadhi Mkuu.

(2) Mtu aliyeteuliwa kuwa Kaimu Kadhi Mkuu atakuwa na mamlaka kama Kadhi Mkuu na atatekeleza kazi zote za Kadhi Mkuu mpaka Kadhi Mkuu atakaporejea katika ofisi au Kadhi Mkuu mpya atakapoteuliwa.

Majukumu ya Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

**18.**-(1) Kadhi Mkuu atakuwa ni Mkuu wa Mahakama za Kadhi ambaye atakuwa na jukumu la usimamizi wa jumla wa Mahakama za Kadhi.

(2) Naibu Kadhi Mkuu atakuwa ni msaidizi mkuu kwa Kadhi Mkuu na atatekeleza majukumu mengine kama atakavyopangiwa na Kadhi Mkuu.

(3) Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu, kabla ya kuanza kazi, watakula kiapo mbele ya Rais.

Muda wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

**19.**-(1) Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu atabakia katika nafasi yake mpaka atakapofika umri wa miaka sitini ambapo anaweza kustaafu kwa hiari, au umri wa miaka sitini na tano ambapo atastaafu kwa lazima.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Rais anaweza kuongeza muda wa Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu kwa kipindi atakachoona kinafaa, lakini kipindi hicho hakitozidi miaka mitano.

Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

**20.**-(1)Mahakama ya Kadhi ya Rufaa itakuwa na Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu na Makadhi wengine wasiopungua watatu wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

(2) Shauri katika Mahakama ya Kadhi ya Rufaa litasikilizwa na Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi mwengine yeyote wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

(3) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Makadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa au mtu mwenye sifa zinazofanana na Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Tume ya Utumishi ya Mahakama itapendekeza kwa Rais majina ya watu ambao wana sifa ya kuteuliwa kuwa Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

(5) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa, kabla ya kuanza kazi, atakula kiapo mbele ya Rais.

Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa.

**21**.-(1) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama kutoka miongoni mwa Makadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Wilaya au mtu mwenye sifa zinazofanana na Kadhi wa Mahakama ya Kadhi wa Wilaya.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa ikiwa mtu huyo:

(a) ni muumini na mfuasi wa dini ya Kiislamu;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya Sharia ya Kiislamu kutoka taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka mitano katika mambo yanayohusiana na Sharia ya Kiislamu; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

(3) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa, kabla ya kuanza kazi, atakula kiapo mbele ya Jaji Mkuu.

Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Wilaya.

**22**.-(1) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Wilaya atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Wilaya ikiwa mtu huyo:

(a) ni muumini na mfuasi wa dini ya Kiislamu;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya Sharia ya Kiislamu kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka mitatu katika mambo yanayohusiana na Sharia ya Kiislamu; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu

(3) Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Wilaya, kabla ya kuanza kazi, atakula kiapo mbele ya Jaji Mkuu.

Mrajis wa Mahakama za Kadhi.

**23**.-(1) Kutakuwa na Mrajis wa Mahakama za Kadhi ambaye atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mrajis wa Mahakama za Kadhi ikiwa mtu huyo:

(a) ameteuliwa kuwa Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa; na

(b) ana uzoefu wa kazi wa angalau miaka mitano katika majukumu ya Mahakama.

(3) Mrajis atasaidiwa na Naibu Warajis ambao watateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama baada ya mapendekezo ya Kadhi Mkuu.

(4) Naibu Mrajis atakuwa na sifa sawa na za Mrajis.

(5) Mrajis, kwa utekelezaji bora wa kazi za Mahakama, atawajibika kwa Kadhi Mkuu.

Majukumu ya Mrajis.

**24**.-(1) Majukumu ya Mrajis wa Mahakama za Kadhi ni:

(a) kusoma hukumu zilizotolewa na Mahakama ya Kadhi ya Rufaa;

(b) kutoa amri na kufanya kazi yoyote ya Mahakama ya Kadhi ya Rufaa ikijumuisha:

(i) kupokea rufaa, marudio au mapitio;

(ii) kutoa na kutuma hati ya wito;

(iii) kuahirisha shauri la Mahakama ya Kadhi ya Rufaa;

(iv) kusikiliza maombi yanayohusiana na malipo ya amri;

(v) kuelekeza kufanyika marekebisho ya maombi ya rufaa, marudio au mapitio; na

(vi) kusimamia malipo ya gharama na utekelezaji wa amri kwa ujumla;

(c) kutekeleza majukumu mengine yoyote atakayopangiwa na Kadhi Mkuu au aliyopewa na sheria nyengine yoyote.

(2) Mrajis wa Mahakama za Kadhi, katika kutekeleza majukumu yake ya kimahakama chini ya masharti ya Sheria hii, atakuwa na uwezo sawa na Mrajis wa Mahakama Kuu katika kesi za madai.

(3) Mtu ambaye hajaridhika na amri yoyote iliyotolewa na Mrajis wa Mahakama za Kadhi anaweza, kupitia ombi litakaloambatana na hati ya kiapo, kukata rufaa dhidi ya amri hiyo katika Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

(4) Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa atakuwa na uwezo, kwa ombi la mtu yeyote aliyeathirika na amri au agizo lililotolewa na Mrajis, kutengua amri au agizo hilo na kutoa uamuzi mwengine au amri itakayokuwa ya haki.

(5) Ombi chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, litafanywa ndani ya siku thelathini baada ya kutolewa amri au agizo au ndani ya muda wa ziada kama Kadhi Mkuu atakavyoruhusu.

(6) Ombi chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, halitatumika kama zuio la kuendelea kwa shauri lolote au ukazaji wa amri yoyote, isipokuwa kama Mrajis wa Mahakama za Kadhi, Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa, kama itakavyokuwa, ataamrisha vyenginevyo.

## SEHEMU YA NNE
## UTATUZI WA MIGOGORO

Uwezo wa Mahakama ya Kadhi kuupeleka mgogoro kwenye utatuzi.

**25.**-(1) Mahakama ya Kadhi ambayo ina mamlaka ya awali ya kusikiliza shauri, wakati shauri lishafunguliwa, na kutokana na ombi la mdaawa au Mahakama yenyewe, inaweza kuupeleka mgogoro kwenye utatuzi.

(2) Utatuzi uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, unaweza kuwa kwa njia ya usuluhishi au upatanishi.

(3) Kadhi Mkuu, endapo itahitajika, atateua wasuluhishi au wapatanishi kwa mujibu wa vigezo na sifa kama itakavyoainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Haki za wadaawa katika usuluhishi au upatanishi.

**26.** Wadaawa wenye mgogoro, wakati wa hatua ya usuluhishi au upatanishi, watakuwa na haki ya kutatua jambo lolote kuhusiana na suala linalojadiliwa katika usuluhishi au upatanishi.

Usiri.

**27**. Mawasiliano yote katika vikao vya usuluhishi, nyaraka na kumbukumbu za usuluhishi yatachukuliwa kuwa ni siri, na baada ya hapo taarifa zozote zilizotolewa wakati wa usuluhishi hazitazingatiwa na hazitatumika kama ushahidi katika mwenendo wa kesi Mahakamani au juhudi nyengine za usuluhishi, isipokuwa kuhusiana na madai yaliyoletwa na mdaawa yeyote kutengua makubaliano ya suluhu kwa sababu ya udanganyifu.

Muda wa usuluhishi au upatanishi.

**28.**-(1) Muda wa usuluhishi au upatanishi hautozidi siku kumi na nne kutoka tarehe ya siku ya kikao cha kwanza cha usuluhishi au upatanishi, na endapo kuna ulazima wa muda wa ziada, muda huo wa ziada utaidhinishwa na wadaawa.

(2) Msuluhishi au mpatanishi atawasilisha muda wa ziada ulioidhinishwa na wadaawa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kwa Kadhi anayeendesha shauri.

Usitishaji wa usuluhishi au upatanishi.

**29**.-(1) Msuluhishi au mpatanishi anaweza kusitisha usuluhishi au upatanishi na kuurejesha mgogoro kwenye Mahakama ikiwa haiwezekani kuendelea na usuluhishi au upatanishi kutokana na kushindwa kwa mdaawa mmoja au wadaawa wote kuhudhuria kwenye mashauri bila ya sababu ya msingi au kutokana na sababu nyengine yoyote iliyo nje ya uwezo wa msuluhishi au mpatanishi.

(2) Mdaawa ambaye hakubaliani na uamuzi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ndani ya siku saba kutoka tarehe ya uamuzi huo ulipotolewa, anaweza kuomba kwenye Mahakama inayohusika na shauri hiyo kurejeshwa tena usuluhishi au upatanishi.

(3) Endapo Mahakama imeridhika kwamba mdaawa ambaye hajakubaliana na uamuzi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ana sababu za msingi, inaweza kurejesha tena usuluhishi au upatanishi.

Kufikia mwisho kwa usuluhishi au upatanishi.

**30**. Usuluhishi au upatanishi utafikia mwisho endapo:

(a) msuluhishi au mpatanishi anasitisha kikao cha usuluhishi au upatanishi ikiwa mdaawa mmoja au wote hawafuati maelekezo au wanavunja misingi iliyokubaliwa;

(b) msuluhishi au mpatanishi, baada ya kushauriana na wadaawa, anatoa tamko kwamba usuluhishi au upatanishi wa ziada hauwezekani wala hauna maana;

(c) wadaawa wameshatekeleza makubaliano ya utatuzi;

(d) wadaawa kwa pamoja wamekubaliana kusitisha usuluhushi au upatanishi; na

(e) mdaawa anatoa tamko kwa msuluhishi au mpatanishi kusitisha usuluhishi au upatanishi na mdaawa mwengine anakubali.

Usajili wa makubaliano ya utatuzi.

**31**.-(1) Mahakama, baada ya kuridhika na makubaliano ya utatuzi baina ya wadaawa, itasajili makubaliano ya utatuzi wa usuluhishi au upatanishi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, makubaliano ya utatuzi yatachukuliwa kama hukumu ya maridhiano, na Mahakama itakuwa na uwezo wa kuitekeleza.

Kushindwa kufikia utatuzi kwa njia ya usuluhishi au upatanishi.

**32**. Endapo usuluhishi au upatanishi umefikia mwisho na hakuna makubaliano ya utatuzi yaliyofikiwa, mgogoro utarudishwa kwa Kadhi ambaye ataendelea na usikilizaji wa shauri kuanzia pale lilipofikia na katika jambo lililopelekea mgogoro kupelekwa kwenye usuluhishi au upatanishi.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Bajeti na fedha za Mahakama za Kadhi.

**33**.-(1) Mahakama za Kadhi zitakuwa na Fungu lake la bajeti ambapo ndani yake zitaingizwa fedha zote zilizoidhinishwa au kupatikana kwa ajili ya matumizi ya Mahakama za Kadhi.

(2) Mlipaji Mkuu wa Serikali atateua afisa masuuli kwa ajili ya Fungu la Mahakama za Kadhi, na Mhasibu Mkuu wa Serikali atateua wafanyakazi wa kufanya kazi ya kiuhasibu kwa ajili ya Fungu hilo.

(3) Fedha za Mahakama za Kadhi zitajumuisha:

(a) kiwango cha fedha kilichoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi; na

(b) misaada, michango na fedha nyengine zinazopokelewa na Mahakama za Kadhi kutoka vyanzo vyengine vinavyokubalika.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

Uwezo wa Mahakama za Kadhi kutilia nguvu fatwa za Mufti Mkuu.

**34**. Bila ya kuathiri masharti ya Sheria ya Mufti Mkuu, Mahakama ya Kadhi itakuwa na uwezo wa kutilia nguvu fatwa yoyote itakayotolewa na Mufti Mkuu, endapo haitotekelezwa.

Uwezo wa kutoa amri ya muda mfupi.

**35**. Wakati wowote ambapo shauri bado linaendelea katika Mahakama ya Kadhi, mdaawa anaweza kuomba amri ya muda mfupi na Mahakama inaweza kutoa amri hiyo au kutoa maelekezo yanayohusiana na ombi hilo ambalo mdaawa ameliwasilisha kama Mahakama itakavyoona inafaa kisheria kwa ajili ya kulimaliza shauri hilo kwa haki.

Mthibitishaji nyaraka na Kamishna wa viapo.

**36** -(1) Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu, Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa au Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa, kwa nafasi yake atakuwa na uwezo na jukumu la mthibitishaji nyaraka na kamishna wa viapo katika mambo ya Kiislamu na atatumia uwezo huo kuhusiana na mambo yafuatayo:

(a) kusimamia viapo;

(b) kuthibitisha saini; na

(c) kuthibitisha nakala za nyaraka.

(2) Ada zitakazotozwa kwa kazi zinazofanywa na mthibitishaji nyaraka na kamishna wa viapo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitakuwa ni sehemu ya mapato ya Serikali.

Mgongano wa maslahi.

**37**. Kadhi hatotekeleza jukumu lake la kimahakama katika shauri lolote ambalo yeye ana maslahi yoyote ya kifedha au binafsi.

Lugha ya Mahakama za Kadhi.

**38**.-(1) Lugha ya Mahakama za Kadhi itakuwa ni Kiswahili.

(2) Endapo yeyote kati ya wadaawa hajui lugha ya Kiswahili au ana ulemavu wa **uziwi** au ulemavu mwengine wowote ambao unamzuia yeye kufahamu lugha ya Mahakama ya Kadhi, Mahakama itaajiri mkalimani.

(3) Mkalimani atakula kiapo mbele ya Kadhi wa Mahakama, kabla hajatekeleza jukumu lake kama mkalimani.

Kudharau Mahakama ya Kadhi.

**39**.-(1) Mahakama ya Kadhi itakuwa na mamlaka ya kuanzisha shauri dhidi ya mtu yeyote kwa kudharau Mahakama ya Kadhi na inaweza, katika shauri hilo, kutaka utekelezaji wa amri au kutoa adhabu.

(2) Mtu ambaye:

(a) ndani ya jengo ambalo Mahakama yoyote shauri linaendeshwa, au katika eneo la jengo hilo, anaonesha dharau kwa maneno au kwa namna yoyote kuhusiana na shauri hilo, au kwa mtu yeyote ambaye mbele yake shauri hilo linaendeshwa;

(b) ameitwa kutoa ushahidi katika shauri, ameshindwa kuhudhuria au amehudhuria lakini amekataa kuapishwa au kuthibitisha, au bila ya sababu ya kisheria amekataa kujibu swali lolote au kuwasilisha nyaraka yoyote, au amebakia kwenye chumba ambacho shauri linaendeshwa baada ya kuamrishwa aondoke kwenye chumba hicho;

(c) anasababisha kikwazo au usumbufu wakati shauri linaendelea;

(d) wakati mwenendo wa kimahakama umesimama, anatumia maneno au maandishi, yanayopotosha shauri hilo au yanayoweza kumuathiri mtu yeyote kwa kumpendelea au dhidi ya mdaawa yeyote katika shauri hilo, au yamekusudiwa kushusha mamlaka ya mtu yeyote ambaye mbele yake shauri linasikilizwa;

(e) anajaribu kinyume na sheria kuingilia au kumshawishi shahidi katika mwenendo wa Mahakama;

(f) amekataa kutii amri ya Mahakama; au

(g) anatenda kitendo chengine chochote cha dharau ya makusudi au kuharibu mwenendo wa shauri, au kwa mtu ambaye mbele yake shauri linasikilizwa,

ametenda kosa la kudharau Mahakama, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyozidi Shilingi Laki Tatu za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja au adhabu zote mbili.

(3) Endapo kosa la dharau limefanywa mbele ya Mahakama, haitokuwa lazima kwa Mahakama kutoa notisi ya kumtaka mtu atoe sababu, lakini Mahakama itahakikisha kuwa mtu huyo anayetuhumiwa kudharau anafahamu aina ya kosa alilotuhumiwa dhidi yake na amepata fursa ya kusikilizwa utetezi wake, na kumbukumbu sahihi za mwenendo wa shauri zitawekwa.

(4) Endapo kosa la dharau limefanywa nje ya Mahakama, notisi ya kumtaka mtu atoe sababu ya kwanini hatua isichukuliwe au shauri lisifunguliwe dhidi yake itatolewa kwa mtu aliyetuhumiwa kutenda kosa hilo.

Kuhudhuria kwa Wakili, Vakili au Wakala.

**40**.-(1) Wakili, Vakili au Wakala aliyeidhinishwa anaweza kuhudhuria kwa niaba ya mdaawa yeyote katika Mahakama za Kadhi au Mahakama Kuu.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Wakili, Vakili au Wakala watatakiwa kuwa na elimu ya uwelewa ya dini ya Kiislamu na watatakiwa kuthibitishwa na Jaji Mkuu.

Kinga ya maafisa wa Mahakama ya Kadhi.

**41**. Afisa wa Mahakama ya Kadhi hatoshtakiwa katika shauri lolote la madai au la jinai kwa kitendo chochote alichokifanya au amri aliyoitoa kutekelezwa wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kimahakama au katika kutumia uwezo wake wa kimahakama ikiwa wakati wa kutekeleza kitendo hicho au kutoa amri hiyo alifanya kwa nia njema.

Kanuni.

**42**. Jaji Mkuu anaweza, kwa kushauriana na Kadhi Mkuu, kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii ikijumuisha utaratibu wa usuluhishi na upatanishi.

Marekebisho ya Jadweli.

**43**. Jaji Mkuu anaweza, kwa kushauriana na Kadhi Mkuu na kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kurekebisha Jadweli la Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**44**.-(1) Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017 inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mambo yote na mashauri yanayoendelea kwenye Mahakama ya Kadhi yataendelea na yatakamilishwa chini ya Sheria iliyofutwa, na mambo yote yaliyofanywa au maamuzi yaliyotolewa chini ya Sheria iliyofutwa, yatachukuliwa kuwa yamefanywa au kutolewa chini ya masharti ya Sheria hii.

**JADWELI**

---

**MAMLAKA YA AWALI YA KIPEKEE**
**[Chini ya kifungu cha 5(1)]**

---

| JAMBO HUSIKA | MAHAKAMA |
|---|---|
| Ndoa, mahari, talaka, kitoka nyumba na mambo mengine yanayohusiana na hayo. | Mahakama ya Kadhi ya Wilaya. |
| Matunzo ya mke. | Mahakama ya Kadhi ya Wilaya. |
| Malezi na matunzo ya watoto. | Mahakama ya Kadhi ya Wilaya. |
| Kafala. | Mahakama ya Kadhi ya Mkoa. |
| Kuthibitisha nasabu. | Mahakama ya Kadhi ya Mkoa. |
| Wakfu,wasia na mirathi. | Mahakama ya Kadhi ya Mkoa. |
| Migogoro kuhusiana na misikiti au taasisi za kidini. | Mahakama ya Kadhi ya Mkoa. |
| Amana za kidini, hiba na misaada. | Mahakama ya Kadhi ya Mkoa. |
| Mgawanyo wa mali ya pamoja iliyochumwa wakati wa ndoa. | Mahakama ya Kadhi ya Mkoa. |

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 30 Novemba, 2023.

.............................................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***